



CHUO KIKUU CHA KENYATTA

IDARA YA KISWAHILI

UTARATIBU WA KUTAYARISHA TASNIFU ZA UZAMILI NA UZAMIFU

Tasnifu zote za shahada ya uzamili na uzamifu zinafaa kutayarishwa na kutahiniwa kwa kuzingatia utaratibu ufuatao:-

- Kusoma kwa mihula mitatu na mwanafunzi awe amepita katika kozi zote.
- Atayarishe makala dhanishi baada ya kushauriana na wahadhiri idarani.
- Makala dhanishi yatiwe sahihi na mwanafunzi pamoja na mwelekezi kisha kuwasilishwa kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Umahiri.
- Wanakamati wa kamati ya Umahiri kuyapitia makala dhanishi na kuteua wasimamizi wawili.
- Mwanafunzi kuanza kuandika pendekezo la utafiti akielekezwa kwa karibu na wasimamizi wake.
- Mwanafunzi kutetea pendekezo la utafiti idarani.
- Mwanafunzi kufanya marekebisho kisha:-
 - kuwasilisha nakala mbili zilizofanyiwa masahihisho idarani
 - nakala ya kumbukumbu za kikao cha utetezi
 - ripoti ya *turnitin*
 - risiti ya malipo yote ya karo.
- Pendekezo la utafiti kutumwa kwa shule ya Umahiri na Mwenyekiti wa idara baada ya pendekezo hilo kutiwa sahihi na wasimamizi wake na mwenyekiti wa idara.
- Shule ya Umahiri kuteua wasimamizi kirasmi.
- Shule ya Umahiri kutoa kibali cha utafiti wa nyanjani kwa mwanafunzi.
- Mwanafunzi pia anahitajika kupata kibali cha NACOSTI cha kumwezesha kufanya utafiti nyanjani.
- Mwanafunzi kuendelea na utafiti akielekezwa na wasimamizi wote wawili.

- Wasimamizi kujaza fomu ya Maendeleo ya Utafiti (*Progress Report*) kila wanapokutana na mwanafunzi..
- Mwanafunzi akimaliza utafiti awasilishe nakala tatu kwa idara, ripoti ya *turnitin* na risiti ya malipo yote ya karo.
- Mwenyekiti wa idara kuteua watahini wawili wa ndani na kutuma majina yao kwa Shule ya Umahiri pamoja na nakala tatu za kazi ya mwanafunzi.
- Watahini wa ndani kupokea tasnifu kutoka shule ya umahiri ili kuitahini.
- Watahini kurudisha tasnifu katika shule ya umahiri.
- Kazi ya mwanafunzi kurudi idarani kutoka kwa Shule ya Umahiri.
- Mwenyekiti kuwapasha wasimamizi kuhusu kurejeshwa idarani kwa kazi ya mwanafunzi
- Wasimamizi kumpasha habari mwanafunzi.
- Mwanafunzi kufanya marekebisho yaliyopendekezwa na watahini wa ndani.
- Wasimamizi kutia sahihi kazi ya mwanafunzi na pia cheti cha masahihisho baada ya kuridhika na masahihisho ya mwanafunzi.
- Mwanafunzi kutayarisha nakala tisa za tasnifu na nakala tatu ororo katika CD zote zilizotiwa sahihi na wasimamizi na kuziwasilisha kwa mwenyekiti.
- Mwenyekiti kuwasilisha cheti cha masahihisho ya mwanafunzi na nakala ya machapisho ya mwanafunzi kwa Shule ya Umahiri.
- Mwanafunzi kusubiri kufanya mawasilisho ya Shule ya Umahiri kwa ajili ya kufuzu.
- Mwanafunzi hatimaye kufuzu na kupata shahada ya uzamili katika somo la Kiswahili.